# MTAALA WA UMILISI

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

STEP FLYER (002) (4)

## GREDI 4 - MWAKA 2023

## SHUGHULI ZA KISWAHILI

***Muda:Saa 1 Dak 40***

**SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

**1.** Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 30.

**2.** Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-

*(i) Jina lako* *(ii) Jina la shule yako* *(iii). Nambari ya Knec*

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 1-5.***

Kabla ya kwanza kufua nguo hakikisha una besheni, sabuni maji safi na mahali pa kwanika. Hakikisha kuwa kuna jua au upepo. Usipange kufua nguo wakati mvua inanyesha. Tenga nguo zinazotoa rangi na zile ambazo hazitoi rangi. Tenga pia nguo chafu sana kutoka kwa zile ambazo si chafu sana usifue soksi na hanchifu pamoja. Soksi huwa na uchafu mwingi.

Mimina maji ya kutosha kwenye besheni. Tia sabuni kipimo kinachotosha, kama ni sabuni ya unga. Koroga maji hadi povu liwe jingi weka nguo zako kwenye besheni ukitanguliza zile nyeupe. Sugua nguo zako taratibu ukiangazia zaidi sehemu zenye uchafu. Sugua mpaka ziwe safi.

**1.** Ni kipi hakihitaji kati ya hivi unapoanza kufua nguo?
A. Sabuni
B. Maji safi
C. Beseni
D. Jokofu

**2.** Ni wakati gani mwafaka wa kufua nguo? Wakati
A. wa mvua
B. wa jua au upepo
C. kuna mawingu
D. kuna jua

**3.** Ni vazi lipi halifai kufulia pamoja na mengine?
A. Soksi
B. Rinda
C. Hanchifu
D. Kaptura

**4.** Kwa nini unafaa kukoroga maji baada ya kuongeza sabuni ya unga?
A. Ili povu liwe jingi
B. Ili kutoa nguo chafu
C. Ili maji yawe safi
D. Ili kupasha maji joto

**5.** Ni sehemu ipi katika nguo inayofaa kusuguliwa zaidi unapofua nguo?
A. Sehemu nyeupe
B. Sehemu iliyo chafu
C. Sehemu yenye doa
D. Sehemu iliyo na rangi

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali 6-10.***

Simba alitangaza nafasi ya naibu wake. Alitaka asaidiwe kuwaongoza wanyama. Ndovu, Sungura, Kobe na fisi walituma maombi yao. Simba aliona bora awape mtihani ili mshindi awe ndiye naibu wake.

"Nina jogoo ambaye hutaga mayai kila siku mlimani. Je, kutakuwa na mayai mangapi baada ya wiki moja?" Simba aliwauliza. Jibu la ndovu lilikuwa mayai saba. Sungura naye alisema mayai matano. Kobe aliandika sufuri huku fisi akiandika mayai kumi na manne.

**6.** Ni mnyama yupi kati ya hawa ambaye hajatajwa kwenye kifungu?

A. Fisi

B. Kobe

C. Sungura

D. Ngiri

**7.** Simba alitangaza nafasi gani katika himaya yake?

A. Msaidizi wake

B. Mpishi wake

C. Naibu wake

D. Mlinzi wake

**8.** Ndovu alitoa jibu lipi?

A. Saba

B. Matano

C. Kumi na manne

D. Sufuri

**9.** Ni mnyama yupi aliyekuwa kiongozi wa wanyama waliotajwa kwenye kifungu?

A. Kobe B. Sungura

C. Simba D. Ndovu

**10.** Je, unafikiria ni mnyama yupi aliyeshinda na kuwa naibu wa Simba?

A. Ndovu B. Kobe

C. Sungura D. Simba

***Soma kifungu hiki kisha ujaze nafasi zilizoachwa wazi 11-19.***

Juma alikuwa mwana ___**11**___ pili katika familia ya Bwana Wanjuma. Mama ___**12**___ aliaga dunia kutokana na ugonjwa wa saratani. Baadaye baba yake akao mke mwingine wa ___**13**___ Juma na watoto wao wengine. Mama wa Kambo alianza kwatesa ___**14**___ baba yao hakujua.

Mateso yalipozidi, Juma___**15**___ kutorokea mtaani na kurandaranda huko. Alikamatwa ___**16**___ polisi na kupelekwa ___**17**___ ili aendelee na masomo yake. Alitia bidii za ___**18**___ masomoni hadi akafuzu ___**19**___ na kujiunga na shule ya upili .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | **A.** ya | **B.** wa | **C.** za | **D.** la |
| **12.** | **A.** yangu | **B.** wao | **C.** yao | **D.** zao |
| **13.** | **A.** kuwalea | **B.** kumlea | **C.** kulewa | **D.** kulea |
| **14.** | **A.** lakini | **B.** kwa | **C.** baina | **D.** kuwa |
| **15.** | **A.** aliamua | **B.** aliamwa | **C.** aliamua | **D.** aliamuliwa |
| **16.** | **A.** za | **B.** mwa | **C.** kwa | **D.** na |
| **17.** | **A.** nyumbani | **B.** kanisani | **C.** mtaani | **D.** mjini |
| **18.** | **A.** sungura | **B.** siafu | **C.** mchwa | **D.** nyani |
| **19.** | **A.** mzura | **B.** vizuri | **C.** nzuri | **D.** zuri |

**_SARUFI_**

**_Kuanzia swali 20-30 jibu kulingana na maagizo_**

**20.** Watu huagana vipi usiku.

A. Tuonane

B. Alamsiki

C. Habari

D. Ndoto mbaya

**21.** Jina **kipofu** liko katikia ngeli ipi?


A. KI-VI

B. I-ZI

C. LI-YA

D. A-WA

**22.** Upande uliochorwa **Z** huitwa ________




A. magharibi

B. kaskazini

C. kusini

D. mashariki

**23.** Neno lilopigwa kistari katika sentensi ni la aina gani? Ngao iko **juu ya** kitanda

A. nomino

B. kitenzi

C. kihusihi

D. kielezi

**24.** **Kanusha.** Mama ananiita

A. Mama aliniita

B. Baba ananiita

C. Mama haniiti

D. Baba haniiti

**25.** **Andika kwa wingi.** Chura ameruka

A. vyura vimeruka

B. vyura hawaruki

C. Chura wameruka

D. Vyura wameruka

**26.** **4004** kwa maneno ni

A. Mia nne na nne

B. Nne elfu na mia nne

C. Elfu nne sufuri nne

D. Elfu nne na nne

**27.** ***Tegua kitendawili.*** Njoo umwone umpendaye

A. Kioo

B. kivuli

C. Picha

D. Mama

**28.** Sisi ______ tuliozawadiwa zaidi.

A. ndio

B. ndisi

C. ndiwo

D. ndiye

**29.** ***Kamilisha tashbihi ifuatayo***

Mweusi kama __________

A. makaa

B. giza

C. shetani

D. ubao

**30.** ***Kamilisha methali***

Haba na haba ___________

A. ndio haba

B. hujaza ndoo

C. hujaza kibaba

D. ndio mwendo

**SEHEMU YA B: INSHA**

| JINA LAKO | |
|---|---|

***Andika insha ya kusisimua kuhusu mada ifuatayo.***

**SHULE YETU**